# Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Siku 16 za Kampeni: **Mwongozo wa Majadiliano ya Mabango**

Mabango ni nyenzo muhimu ya mawasiliano. Hii ni kwa sababu inajimuisha na watu wa aina mbalimbali bila ya kujali viwango vyao vya elimu. Kama nyenzo ya mawasiliano yenye ufanisi kwa kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake bango pia linaweza kutumika kama chombo cha kushirikisha jamii. Kabla ya kuonyesha mabango unaweza kushirikisha vikundi vidogo vya watu katika mijadala ya mada iliyopo katika mabango. Tumia maswali nyuma ya kadi hii ili kuongoza mjadala wako kuhusu siku 16 kwa kutumia bango la mwaka huu lenye kauli mbiu: Paza Sauti Chukua Hatua - Sasa! Ongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake.

## Vidokezo vya majadiliano ya mabango

1. Majadiliano ya kikundi yanapaswa kuwa na kiwango kisicho zidi watu 15 ili kuwa ya maana. Inaweza kufanyika katika mazingira yoyote ndani ya jamii ambapo watu wanaweza kukusanyika na kuzungumza, kwa mfano chini ya mti, nje ya nyumba ya mtu, katika saluni, katika baa.
2. Waeleze washiriki kwamba hakuna majibu yaliyo sahihi au sio sahihi. Washukuru washiriki kwa michango yoyote itakayotolewa.
3. Kumbuka kwamba maswali haya ni mwongozo tu. Huna haja ya kuyasoma kama mswada au kwa kufuata utaratibu uliyo sahihi. Jaribu kufanya mazungumzo kuwa ya kawaida na chokoza mjadala kwa undani zaidi pale inapobidi.
4. Himiza uchangiaji kutoka kwa washiriki wote, kuwapa fursa sawa ya kushiriki.
5. Kumbuka usiwaambie washiriki nini cha kufikiri. Kuuliza maswali kunaweza kuwa na nguvu zaidi kuliko kutoa ujumbe.
6. Baada ya kukamilisha majadiliano, bandika bango katika eneo lililo wazi kwa kundi hilo.

## Mapendekezo ya Maswali ya Majadiliano

1. Je, unaona nini katika bango? Una elewa nini?
2. Ni kwa jinsi gani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana unakuwa ni kikwazo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii yako?
3. Jinsi gani unaweza kuwafanya viongozi wenu (yaani wa dini, jamii, kimila, kisiasa na wataalamu) kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana?
4. Ni hatua gani nyingine unadhani viongozi katika jamii yako wanapaswa kuchukua ili kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana?
5. Ni hatua gani utakazochukua ili kuhakikisha viongozi wanachukua hatua kama ulivyoelezea katika swali la 2 na 3 hapo juu?
6. Ni jinsi gani utaongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake?



GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum • Fostering Activism